HakiElimu
Brief Na.06.3K

# Hali ya Kazi na Maisha ya Walimu Tanzania

## Matokeo ya Ripoti ya Utafiti

Hii ni muhutasari wa ripoti ya utafiti wa 2004, "Hali ya Kazi na Maisha ya Walimu Tanzania" (ISBN 9987-423-13-2) iliyotolewa na HakiElimu na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

**Kwa nini utafiti huu?**

Tangu serikali ya Tanzania ilipoanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2001, maendeleo makubwa yamefanyika kuhusiana na ongezeko la upatikanaji wa elimu ya msingi. Hata hivyo, kuboresha elimu inasalia kuwa changamoto ya msingi. Mojawapo ya vigezo muhimu kabisa vinavyoathiri ubora wa elimu ni ubora wa walimu. Utekelezaji fanisi wa MMEM hauwezi kufanyika bila ya uelewa bayana wa jinsi ya kuwavutia na kuwafanya walimu bora wabakie katika ualimu. Utafiti huu ulifanywa ili kupata maoni ya utambuzi wa walimu wenyewe kuhusu hali yao ya maisha na ya kufanyia kazi, ili kusaidia kuiboresha hali ya elimu kwa jumla.

**Methodolojia**

Utafiti huu ulibuniwa na kutekelezwa na mtafiti anayejitegemea, kwa niaba ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT), kwa msaada wa uchanganuzi wa HakiElimu. Taarifa zilikusanywa kutoka kwenye wilaya moja ndani ya kila mojawapo ya kanda saba za kielimu Tanzania: Ilala, Manyoni, Manispaa ya Moshi, Kibondo, Jiji la Mwanza, Ludewa na Lindi Vijijini. Utafiti huu unatoa maoni kutoka kwa walimu kutoka mtawanyo mkubwa wa mazingira ya kijamii-kiutamaduni. Katika kila wilaya, shule tatu za msingi na mbili za sekondari (moja binafsi na moja ya umma) ziliteuliwa kwa uchanganuzi.

Hojaji (questionnaire) zilisambazwa kwa walimu ili kupata data ya wingi. Zaidi ya hayo, data ya ubora ilipatikana kupitia mahojiano binafsi na walimu walioteuliwa. Walimu waliteuliwa kwa ajili ya usaili kwa msingi wa jinsia na sifa zao, ili kuwakilisha kiusahihi muundo wa wafanyakazi wafundishaji. Jumla ya mahojiano 74 ya walimu wa shule za msingi na 35 ya walimu wa shule za sekondari yalifanyika, na walimu 1,383 wengine walishiriki kwa kujaza hojaji. Pale ilipowezekana, utafiti ulifanya ufananisho na utafiti wa aina hii hii uliofanyika 1991.

**Matokeo Muhimu**

***Heshima:*** Mwelekeo mmoja unaoonekana tangu 1990 ulikuwa ni upunguaji dhahiri katika heshima, inayoambatanisha na taaluma ya ualimu. Mahojiano yalibainisha kwamba walimu wengi, hususani wale walio katika shule za sekondari, walihisi kwamba taaluma yao ilikuwa haiheshimiwi na jamii. Walimu katika maeneo ya vijijini, ambako watu wachache wana mapato ya uhakika, walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kuhisi kwamba taaluma yao ilikuwa inaheshimiwa. Hata hivyo, wahojiwa wengi walisema kwamba walikuwa walimu kama kimbilio lao la mwisho, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 1.

**Jedwali 1: Utambuzi wa Walimu wa Taaluma Yao**
(Mwitikio kwa maswali teule ya mahojiano)

| Swali ya Mahojiano | Ndiyo | Hapana | Hakuna Mwitikio |
|---|---|---|---|
| Je, walimu wanaheshimiwa? | 69.5% | 18.0% | 12.5% |
| Je, utauacha ualimu kama ukipata kazi nyingine? | 50.9% | 37.9% | 11.8% |
| Ungemshauri mwanao awe mwalimu? | 40.3% | 41.9% | 17.7% |

Kwa ujumla, kiasi cha theluthi moja ya walimu walisema wangetafuta kazi nyingine kama wangelipata uwezekano wa kufanya hivyo. Asilimia 40 walisema hawangewashauri watoto wao kufanya kazi ya ualimu.

***Mishahara:*** Huku kupungua katika hadhi ya kijamii kuna uwezekano wa kuakisi kushuka kwa hali yao ya maisha, kama inavyoshuhudiwa kwa mishahara yao. Utafiti huu uliona kwamba mwalimu wa Daraja 1A anapata kiasi cha shilingi 70,000 kwa mwezi, kiasi ambacho karibu kila Mwalimu (97% ya walimu wote) alithibitisha kuwa kilikuwa hakitoshi hata kidogo. Hivyo haishangazi kwamba robo yao walisema kwamba wanalazimika kufanya shughuli nyingine ili kufidia kipato.

***Hali ya Maisha:*** Walimu pia waliripoti wasiwasi wao kuhusu upungufu wa nyumba za walimu, mapungufu

katika mpango wa bima ya afya unaotekelezwa na serikali, matatizo katika kuhamishiwa kwenye shule nyingine, ucheleweshaji katika upatikanaji wa mishahara, na ukweli kwamba walimu wanalazimika kusafiri hadi kwenye ofisi ya Halmashauri ya Wilaya kuchukua mishahara yao, safari ambayo mara nyingi unakuwa ndefu na ghali kwa walimu wa maeneo ya vijijini.

***Uwingi wa wanafunzi:*** Ukusanyaji wa data ya wingi ulidhihirisha kwamba walimu hutumia wastani wa saa 16 kwa juma wakifundisha, muda ambao ni mdogo ikilinganishwa na nchi zinazofanana. Hata hivyo, wengi wa wasailiwa waliripoti kuwa na mzigo mkubwa wa kazi, hasa wale walio katika shule za vijijini. Pengine, kwa kiasi, hili linatokana na walimu kulazimika kutumia muda mwingi kusahihisha kazi za wanafunzi, kwa kuzingatia ukubwa wa madarasa. Ukubwa wa darasa pia unaweza kuchangia ukweli kwamba idadi kubwa (karibu 90%) ya walimu sampuli waliunga mkono adhabu ya viboko.

Madarasa makubwa pia huchakaza rasilimali chache zilizopo za kujifunzia, hususan vitabu vya kiada. Asilimia mbili tu ya walimu waliosailiwa walisema shule zao zilikuwa zinajitosheleza. Hali hizi za kufanyia kazi zina uwezekano mkubwa wa kuwa na athari hasi kwenye ubora wa elimu.

***Upungufu wa Walimu:*** Zikiwa zinakabiliwa na matatizo kama hayo, ugunduzi kwamba shule zilizotumiwa kama sampuli kwa kiasi kikubwa, zimeshindwa kuvutia walimu wenye sifa za hali ya juu haushangazi. Kwa kiasi fulani, ukosefu wa walimu wenye sifa unaturudisha nyuma kwenye enzi za 'UPE' (sehemu ya jitihada za Elimu ya Msingi kwa Wote).

Sifa za ualimu zilijalizwa na kozi za mafunzo hayo, wasailiwa pia walilalamika kutokupewa maelezo ya kutosha kuhusu mabadiliko ya mtaala. Zaidi ya hayo, walimu wengi hawakuandaliwa vizuri kufundisha mada muhimu kama VVU/UKIMWI au kutekeleza mtaala wa mafunzo ya ufundi ("Stadi za Kazi").

**Mapendekezo**

Kufuatana na utafiti huu, hadhi na hali ya kufanyia kazi walimu hawahisi jukumu lao muhimu katika kuboresha ubora wa elimu na kulijenga taifa. Kuanza kuboresha ubora wa elimu katika Tanzania ni muhimu kwamba Serikali (hususani Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi), CWT na AZISE watilie maanani matokeo ya utafiti huu na kufanya kazi kuboresha hali ya maisha ya walimu na mazingira ya kufanyia kazi. Baadhi ya mapendekezo mahususi kwa kila mhusika yameandikwa hapa chini:

***Serikali:***

- Bainisha idadi inayohitajika ya saa za kufundisha kwa juma.
- Anzisha motisha kuwavutia walimu, hasa walimu wanawake wa Daraja A kufanya kazi katika mikoa, wilaya na shule zilizo "ngumu" au za pembezoni.
- Hakikisha kwamba mishahara ya walimu inalipwa kwa muda na katika hali ya kifanisi, bila ya walimu kulazimika kusafiri kwa shida.
- Rekebisha mfumo wa bima ya afya kiasi kwamba walimu wanalazimika kununua dawa kwa sababu hazipo kwenye vyombo vya serikali wanalipwa.

***CWT:***

- Endelea kutetea mishahara ya haki;
- Waeleze walimu wote juu ya haki zao na wajibu wao;
- Toa nafasi kwa ajili ya viwango vikubwa zaidi vya ushiriki wa walimu katika kuendeleza mihutasari na sera ya shule
- Toa taarifa ya mwaka, ukisisitiza mafanikio makuu na mapungufu na isambaze kwa walimu wote.

***AZISE:***

- Jumuisha kero za walimu katika kazi ya utetezi
- Tawanya taarifa juu ya sera kwa shule
- Saidia katika kujenga uwezo wa na kufanya shughuli ya pamoja na CWT.

---

*Imeandikwa na Katherine Manchester na Ruth Carlitz, kutafsiriwa na Saifu Kiango, na kuhaririwa na Hebron Mwakagenda.*

HakiElimu inawezesha wananchi kuleta mabadiliko katika elimu na demokrasia.

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org